



## Kanuni Zetu (kwa Kiswahili)

kutafsiriwa na Katrina Daly Thompson

1. **Utambulisho:** Tunamkulali kama Mwislamu mtu ye yote anayejitambulisha hivyo. Ukweli na uhakika wa dai lake uko kati ya mtu huyo na Mwenyezi Mungu, na si jambo la serikali wala jambo ambalo mtu mwingine anaweza kuhukumu.
2. **Usawa:** Tunathibitisha thamani sawa ya binadamu wote, bila ya kujali ukabila, jinsia, utaifa, dini, wanaowapenda, au uwezo. Tumeweka nia ya kupigania majamii ambayo yatawahakikishia wote nafasi za kijamii, za kisiasa, za kielimu, na za kiuchumi.
3. **Utengano wa Wakuu wa Dini na wa Serikali:** Tunaamini kwamba uhuru wa mawazo ni lazima kwa majamii yote na, zaidi ya hayo, ni sehemu muhimu sana katika jinsi Qur'ani inavyoonyesha hali ya binadamu. Tunaamini kwamba serikali isiyo ya dini ni njia pekee ya kutekeleza wazo la Kiislamu kwamba watu wana uhuru katika masuala ya dini.
4. **Uhuru wa Kutoa Maoni:** Tunatetea uhuru wa kutoa maoni na uhuru wa kugoma, ikiwa katika masuala ya kisiasa, ya kisanaa, ya kijamii, au ya kidini, hata ikiwa maoni hayo yanawasumbua watu au mgomo huo unafikiriwa kumpeleka mtu nje ya Uislamu. Mtu asishtakiwe kisheria, asipelekwe gerezani, wala kuchukuliwa kwa sababu ya kutoa au kukubalia maoni yasiyopendwa na jamii.
5. **Haki za Binadamu Wote:** Tunathibitisha nia yetu ya kupigania haki za kijamii, za kiuchumi, na kimazingira. Tunaamini kwamba uwezo wa watu wote wa kuwa wakamilifu, katika ulimwengu wa usalama na unaoweza kujiedeleza, ni lazima kwa ajili ya uhuru, ustaarabu, na usalama. Tunaunga mkono juhud za kupigania matibabu kwa kila mtu, elimu kwa kila mtu, kuhifadhi mazingira yetu, na kuondoa umaskini.
6. **Haki za Wanawake:** Tunatetea uwezo wa wanawake wa kujitegemea na kujiamulia katika kila sehemu ya maisha yao. Tunaaminia nafasi ya wanawake katika kila sekta ya jamii. Tunathibitisha nia yetu ya kupigania haki za kiuzazi na kuwawezesha wanawake wafanye uamuzi wa afya kuhusu miili yao, mapenzi yao, na uzazi wao.
7. **Haki za Mahanithi, Mashoga, Mabasha, Wasagaji, Magei, na kadhalika:** Tunakubalia haki za kisheria na kibinadamu za wasagaji, magei, mahanithi, mabasha, na watu wote wenye jinsia ambayo ni tofauti na kawaida. Tunatetea usawa kamili na nafasi kwa kila mtu, bila ya kujali anavyofanya mapenzi au anavyoonyesha jinsia, katika jamii na katika umma wa Waislamu. Tunathibitisha

- nia yetu ya kuondoa ubaguzi unaotegemea jinsi mtu anavyofanya mapenzi au kuonyesha jinsia yake.
8. **Ufanuzi na Utafsiri:** Tunatoa mwito kwa watu kusoma kwa makini na kufafanua Qur'ani, hadithi, sheria, na maandishi ya kisasa kuhusu Uislamu. Tunaamini kwamba kufikiri kwa mawazo mapana ni muhimu sana ili tuendelee kidini. Tunaunga mkono ufanuzi wenyewe msingi wa mawazo ya ubinadamu, ujamaa, huruma, na usawa, mawazo ambayo ni msingi wa Qur'ani yenyewe.
  9. **Huruma:** Tunathibitisha kwamba haki na huruma ziwe miongozo kwa kila tendo la watu. Tunakataa mapigano, yakiwa kati ya watu, mashirika, wala mataifa.
  10. **Umbalimbali:** Tunakaribisha umbalimbali wa dini na wa mawazo yanayowapa wato moyo wa kupigania haki za jamii. Tunaamini kwamba dini ya mtu si chanzo pekee cha ukweli. Kwa hivyo, tutatumia vyanzo mbalimbali vya falsafa na vya dini ili kupigania uliwengu wenyewe haki na usalama zaidi na unaoweza kujie ndeleza.